

وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ مَأْمَنُوا إِنَّكُمْ وَعَلَيْكُمُ الْقَدْرُ الْجَاهِدُ لِيَسْتَغْفِرُنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا أَسْتَخْلَفُ
الَّذِينَ مِنْ قَلْبِهِمْ وَلَا يُسْكِنُهُمْ هُنَّ دِيَمْهُمُ الْأَوَّلُ أَرْتَهُمْ فَمُمْ وَلَيْسَ لَهُمْ مِنْ بَعْدِ حَوْفِهِمْ أَنْتَ
يَعْبُدُونِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَنْ كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ



Toleo: 1445 / 05

Jumamosi, 6 Ramadhan 1445 H

16/03/2024 M

Taarifa kwa Vyombo vya Habari

Kampeni ya Ramadhan ndani ya Tanzania

(Imetafsiriwa)

Jana Ijumaa 05 Ramadhan 1445 H / 15 Machi 2024 M wanaharakati wa Hizb ut Tahrir Tanzania katika baadhi ya maeneo walifanya Kampeni Maalum ya Ramadhan chini ya kauli mbiu ya 'Ramadhan ni Kielelezo cha Umoja wa Ummah'

Maandamano baridi yalifanywa katika jiji la Dar es Salaam na Zanzibar, ambapo ndani ya Dar es Salaam yalifanyika nje ya Masjid Dar us Salaam, Kigamboni, pia yalifanyika nje ya Masjid Idrissa, Kariakoo. Kwa Zanzibar maandamano baridi yalifanyika eneo la wazi karibu na Soko la Darajani.

Kampeni ilifafanua bayana kwamba mwezi wa Ramadhan unawasilisha umaja wa Ummah wa Kiislamu kuwa kitu kimoja, wenye shakhsiya moja, pia wenye muongozo mmoja, ambapo kutokana na muongozo huo ndio imepatikana amri hiyo ya Swaumu ya Ramadhan.

Hata hivyo kampeni hiyo iliwhadharisha Waislamu kwamba umaja wa Kiislamu haupaswi kujifunga katika masuala ya ibada za kiroho tu, bali lazima umaja huo utanuke kwa upana hadi kuwa ni umaja wa kisiasa chini ya dola ya kilimwengu ya Khilafah ambayo itasimamia mambo ya Waislamu.

Kuweza kuufikia umaja wa aina hiyo (wa kisiasa) kampeni imewahamasisha Waislamu kushiriki kikamilifu katika jukumu la kurejesha tena dola ya Khilafah kwa Njia ya Utume inayopaswa kuanzia katika ulimwengu wa Kiislamu. Kwa dola hiyo umaja wa kweli wa kisiasa utafikiwa na utaweza kuhifadhiwa.

Masoud Msellel

Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari

Hizb ut Tahrir Tanzania